**LEARNING BY EAR**

# ”If a tree falls… - The Rocket Stove"

## EPISODE FOUR: "Trees and Rainfall"

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

**List of characters EPISODE FOUR:**

**Narrator**

| | | |
|---|---|---|
| **SCENE 1** | **Chika (f, 18)** | |
| **SCENE 2** | **Mulogo (m, 22)** | **Chika (f, 18)** |
| **SCENE 3** | **Mother (f, 36)** | **Talib (m, 20)** |
| **SCENE 4** | **Talib (m, 20)** | **Chief (m, 40)** |
| **SCENE 5** | **Akiki (f, 7)** | **Isi (m, 18)** |

## INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na kipindi cha nne cha mchezo wetu mpya wa redio kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Chifu Apaloo anataka kuwashawishi kina mama wajaribu jiko jipya ambalo amelitengeneza. Wakati huo huo, Chika anafikiria mbinu za kutumia kumkomesha Mulogo asipoacha kumsumbua kimapenzi.

**Episode FOUR: <u>"Rocket Stove."</u>**

**1.MUSIC UP**

**Scene 1**

**2. SFX Day time sounds - outside**

**3.CHIKA NARRATOR:** Huyo Mulogo simwelewi mimi. Mawazo yake na yangu sawa na mbingu na ardhi- anapendekeza mambo yasiyoyumkinika-kujenga mtambo wa umeme na bwawa pamoja na hifadhi ya maji! Sasa, hivyo vyajengewa nani? Wafanyi biashara ya mbao ili waendesha biashara zao na kuharibu misitu zaidi? Na zaidi ya hayo, kila wakati ananipiga kwa vijineno vyake. Njia tu ya yeye kuniacha ni kumkomesha ili asiwahi kunikaribia. Ndo sababu nilimwomba aandamane nami tukatembee. Niliendelea kuzungumzia mada niipendayo sana: Kuhifadhi miti...

**Scene 2**

**3a. SFX Day time sounds - outside**

**4.MULOGO:** Aaakh Chika! Usijisumbue! Tukae chini hapa tuimbe wimbo wako uupendao! (**Laughing)** Unaimba vizuri sana! Nimeshawahi kukusikia!

**5.CHIKA:** Unasema "Don't worry, be happy"? **(singing)** Maanake tukate misitu wala tusijali mabadiliko ya hali hewa duniani, Mulogo? Mwenzangu hujapevuka!

**6.MULOGO:** Unasema kuna uhusiano. Siuoni. Naam, hali ya hewa inabadilika, lakini nani kasema ni kwa sababu yetu sisi kukata miti?

**7.CHIKA:** Si hilo tu…Bila shaka, magari, viwanda vikubwa na uchomaji kuni, yote hayo yanachangia.

**8.MULOGO:** Wajua- Ni lazima tufyeke misitu. Tunahitaji kula. Unafikiria kwamba hali ya hewa huimarishwa pia watu wanapokufa njaa?

**9.CHIKA:** Hilo si jambo la kusema. Unaona kama kwamba mimi ni mtu wa kufurahia watu waangamie? Hutaki kuelewa mambo- tukikata miti tunaongeza kiasi cha gesi ya “carbon dioxide” hewani.

**10.MULOGO:** Hayo nayajua. Miti hufyonza gesi za sumu nalo jua husaidia kuzibadilisha gesi hizo kuwa hewa safi.

**11.CHIKA:** Ndiyo!

**12.MULOGO:** Ukataji miti huongeza vipi gesi za sumu? Hilo limethibitishwa?

**13.CHIKA:** Naam, tena kwa hoja nzito. Viwango ya gesi aina ya “carbon dioxide” vimepanda kwenye miji yetu na miti ya kuifyonza ni michache. Hivyo basi tunazidi kupata kiasi kikubwa cha gesi za sumu.

**14.MULOGO:** …ziitwazo kwa kimombo ‘greenhouse gases’.

**15.CHIKA:** Ndio… Kumbe unayajua yote haya! Unanipotezea wakati bure!

**16.MULOGO: (impatiently)** HAYA lakini nani kasema kwamba sisi binadamu hatuna njia za kujirekebisha? Tumewahi kuyarekebisha maisha yetu yawiyane na hali nyingine za maisha. Au siyo?

**17.CHIKA: (raising her voice)** Basi kati yangu na wewe nani anabeza mambo? Unataka tuishi dunia ya aina gani? Isiyokuwa na miti? Wataka ushahidi, tazama Mlima Elgon. Si mimi ninayetaka watu wafe njaa. Tukiendelea kukata miti kiholela mimea yetu ya mazao itaangamia ama kwa ukame au mafuriko.

**18.MULOGO:** Lakini Ulaya hakuna miti mingi wala hatuwaoni wakifa njaa. Ni njama zao za kutubakisha masikini na wategemezi wa uchumi wao.

**19.CHIKA:** Bara la Ulaya haliko karibu na msitari wa istiwai. Hawana misitu ya mvua. Hali yao ya hewa ni ya wastani na wana mvua nyingi. Na wao pia wameshaanza kupata mafuriko na pia upungufu wa maji. Marekani pia. Barani Afrika tunapoteza maji mengi kutokana na joto, lakini misitu yetu husaidia kuyarejesha tena maji hayo. Bila miti maisha yetu yako hatarini.

**20.MULOGO:** Tunahitaji kuunganisha vijiji vyetu na vituo vya umeme na miji. Hatuwezi kuyamudu maisha tu kwa kung’ang’ania maisha ya porini.

**21.CHIKA:** Unataka kuwahamisha mamilioni ya watu kutoka kwenye misitu? Kwa nini? Maisha ya mjini? Ebu twambie! Kuna nini?

**22.MULOGO:** Barabara, maduka, nyumba nzuri za makazi.

**23.CHIKA: (loud)** Huoni mitaa ya mabanda? Watu wa vijijini, zaidi ya milioni 14, wote wanabanana kwenye miji yetu mikuu barani Afrika. Wanaishi kwa kuchokora majalala ya taka. Maanake maisha ya mkono mdomoni.

**24.MULOGO: (gently)** Tulia, Chika! Usijiumize roho bure! Wewe ni mrembo sana. Una uwezo wa kupata kazi yoyote utakayo. Mbona ufanye kazi kwenye kambi ya wakimbizi?

**25.CHICKA: (softer)** Ai! Mulogo! Ninaipenda kazi hii. Samahani kama nimekukemea. Naona umuhimu wa miti. Zamani bara la Afrika lilikuwa na miti mingi, mimea, wanyama na maua. Vyote hivyo vinatoweka...katika enzi tunayoishi. Tunahitaji hewa safi, maji safi, kuni, dawa na makazi. Vyote hivyo vinatokana na miti. Tunapaswa kuitunza miti yetu. Ebu tazama kila mahali uone jinsi miti inavyotufaa. Njoo. Jitahidi kuwa na akili pevu.

**26.MULOGO: (laughing)** Nitajaribu. Hata hivyo una kibarua kikubwa cha kunishawishi mimi! Tena faraghani!

**<u>27.MUSIC UP</u>**

**Scene 3**

**28. SFX Daytime Outside / Babies/children crying**

**29.MOTHER:** Watoto kumi zaidi wameangamia kwa maradhi ya kuharisha, Talib. Chemchemi za maji zimechafuliwa. Tunahitaji kujua ni zipi zilizochafuka kisha tuzizingire.

**30.TALIB:** Mimi na kundi la vijana tumepanga kwenda kuchukua kiasi fulani cha maji. Kisha tutayafanyia uchunguzi kwenye maabara yetu ndogo. Tutayarishe mabango ya kuwatahadharisha watoto wasicheze na kunywa maji mahali ambapo ng’ombe wapo. Aah! Shirika la *Saidia Afrika* limefadhiliwa kwa fedha za kuchimba kisima kipya cha maji. Tutashiriki sote kukiandaa kisima hicho. Hizi hapa picha zinazoonyesha jinsi kitakavyokuwa.

**31.SFX PAPER NOISE**

**32.MOTHER:** Raha iliyoje! – maji safi kutoka kwenye bomba. Lakini huenda watu watayatumia vibaya.

**33.TALIB:** Ndo maana kabla ya kuyaunganisha tunataka kuwahamsisha watu jinsi ya kutumia maji vyema na kuyahifadhi. Shughuli hiyo inahusiana moja kwa moja na kazi yetu ya kuhifadhi misitu..

**34.MOTHER:** Talib! Napendezwa sana na kazi ambayo wewe na Chika mnafanya. Mnanifungua macho zaidi kuyaangaza vyema mazingira yangu. Si tu mbio za kutafuta riziki kwenye ardhi. Ardhi nayo inahitaji pia kutunzwa irejee kama zamani.

**35.TALIB:** Chifu Apaloo anasema vivyo hivyo.

**36.MOTHER:** Ai! Chifu Apaloo. Nadhani kila anaponiona anamkumbuka tu mume wangu. Walikorofishana kuhusiana na haki za ardhi.

**37.TALIB:** Ndiyo, najua lakini hapa jamaa wanakuheshimu sana. Unawahamasisha kina mama wengi pia. Umekuwa mfano wa kuigwa! Nadhani hata Chifu Apaloo anajua hilo. Hata umenikumbusha., aliniomba nimtembelee nyumbani kwake. Tafadhali waongoze kina mama wengine mtayarishe mabango na muyabandike kwenye vyanzo vya maji. Tutaonana baadaye!

**38.MUSIC UP**

**Scene 4**

**39. SFX Children playing outside, goats /cows**

**40.TALIB: (excited)** Loo! Kazi nzuri sana hii.

**41.CHIEF APALOO: (proudly)**Naam- Ni jiko lisilotumia kuni nyingi. Nimeliunda mimi binafsi.

**42.TALIB:** Alaa! Ebu nionyeshe jinsi linavyofanya kazi.

**43.CHIEF APALOO:** Ndiyo – Kwanza nasisitiza kwamba halina gharama nyingi – mtu hutumia tu vitu vya kienyeji– hakuna kinachoagizwa kutoka nje.

**44.TALIB:** Naona. Una matofali na pipa la chuma,- aaa ni ndoo nzee–mm- vitu hivyo vinapatikana popote.

**45.CHIEF APALOO:** Ndo hivo. Sasa **(Breathing with a groan as he bends down)** Ai! Mwili wangu – mimi si yule wa zamani tena!

**46.TALIB: (laughing)** Acha hayo nawe! Wewe SI mzee! Unatakikana kujiunga nami kila siku asubuhi ninapofanya mazoezi ya kukimbia! Nyinyi machifu mmezoea starehe!

**47.CHIEF APALOO: (laughing)**Hivyo ndivyo unavyofikiri! Sasa basi... unyaona matofali haya sita?

**48.TALIB:** Naam

**49.CHIEF APALOO:** Yatosha kuunda umbo la nusu duara **(breathing heavily as he bends)** Kama hivi. unaona?

**50.TALIB:** Naam.

**51.CHIEF APALOO: (Speaking slowly as he demonstrates)** Sasa, nitaliweka hili pipa... kama hivi...kwenye matofali. Na...hili... linaingia kwenye jiko...kama chemni. Unaona! Limetengenezwa kwa dongo jekundu ambalo linahifadhi joto na pia jepesi...Sasa...

**52.SFX Dried grass**

**53.CHIEF APALOO: (slowly)**Hizi kuni hapa…..majani makavu na nyasi. Nitaziweka hapa kwenye tundu hili kubwa. Unaona tundu hili dogo huku chini?

**54.TALIB:** Naam.

**55.CHIEF APALOO:** Hapo ndipo hewa inapoingilia. Sasa...

**<u>56.SFX rustle of sticks / strike of match</u>**

**57.CHIEF APALOO**: Ninaweka vijiti na majani juu ya nyasi. Tazama – ndimi za moto zimedhibitiwa vizuri.

**58.TALIB:** Na moto nao umedhibitiwa vizuri ndani ya pipa.

**59.CHIEF APALOO:** Ndiyo hivyo,maanake hatuhihaji kutumia kuni nyingi. Ebu tuuache uwake kwa muda kidogo ili tupate joto zaidi.

**60.TALIB:** Pipa juu ya matofali... linafanana na komboro dogo!

**61.CHIEF:** Naam. Jiko la kombora! **(laughing loudly, then dropping his voice)** Lakini kusema kweli, sijalivumbua jiko hili! Majiko aina hii yanauzwa kwenye soko la Abanto!

**62.TALIB:** Ahaa! Kwa hivyo tayari lina hataza. Maana hatuwezi kuyatengeneza na kuyauza!

**63.CHIEF: (more cheerily)** Hapana! Lakini tunaweza kuyatengeneza haya tutumie sisi wenyewe! Hili jiko ndilo nilikuwa nikitaka kukuonyesha! Linaokoa asilimia 50 ya kuni. Hivyo misitu yetu inafaidika.Ama sivyo?

**64.TALIB: (Triumphant)** Asante sana. Hongera! Acha nende nikalete maji. Huu moto haupotei bure. Bora tupike chai!

**<u>65.MUSIC UP</u>**

**Scene 5.**

**66.SFX Evening sounds outside. Dog barking in the distance**

**67.AKIKI: (excited)** Isi. Lori laja! Nasikia mbwa wakibweka kwa mbali. Tazama – wingu la vumbi hilo.

**68.ISI: (over excited)** Kalamu yangu i wapi? Akiki – karatasi zangu…na viatu je… viko wapi **(panting heavily).** Tukimbie. Mimi na Chika tunatakikana kusajili watu wapya. Na je Kato akiwepo? Nitafurahi kiasi cha kushindwa kuandika majina! Tayari ninatetemeka! Haraka.. Fanya bidii!

**69.AKIKI: (breathless)….** Isi! Tafadhali..Nisubiri!

**70.MUSIC UP**

**OUTRO.**

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho “Mti unapoanguka...”, kilichoandikwa na Romie Singh, kinachoshughulikia suala la uharibifu wa misitu.

Katika kipindi chetu kijacho, Akiki anagundua siri fulani kumhusu dada yake na pia ndugu pacha wa Isi. Pia tutatizama maumbile. Kwa mengi zaidi jiunge nasi kwenye kipindi chetu cha tano.

Kumbuka, ikiwa unataka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

**END OF EPISODE FOUR**